

Maswali na Majibu

1. Mbona Farao aliwafanya Waisraeli kuwa watumwa?
Walikuwa wengi sana. Aliogopa kwamba wanaweza kuleta vita nao.
2. Farao aliamrisha watoto wavulana wa Waisraeli wafanyiwe nini?
Lazima watupwe ndani ya mto.
3. Nani aliokoa mtoto Mwisraeli aliyekuwa kwa kikapu kando ya mto. Alimwita yule mtoto eti nani?
Binti Farao. Alimwita Musa.
4. Mbona Musa alitoroka akaenda nchi ya Midiani? Alifanya kazi gani kule?
Kwa sababu alikuwa amemuua Mmisri. Alikuwa mchungaji.
5. Musa aliishi Misri kwa muda gani? Alijifunza nini kama mwana wa mfalme?
Kwa miaka 40. Alijifunza kuwa kiongozi.
6. Mungu aliambia Musa nini kutoka kwa kichaka kilichokua kikiungua?
Jina la Mungu ni MIMI NDIMI. Yeye ni wa milele na ana watu wake kila wakati. Mungu alikuwa amemchagua Musa awaongoze Waisraeli kurudi kwa nchi yao ya ahadi.
7. Farao alisema nini Musa alipomuuliza aachilie Waisraeli waende?
Alisema Hapana. Alikasirika na kuwafanyisha kazi ngumu zaidi.
8. Tauni ya kwanza yenye Mungu alituma Misri ilikuwa gani?
Mto wa Naili ulikuwa damu
9. Tauni zingine nane zenye Mungu alileta Misri zilikuwa gani?
Vyura, chawa, mainzi, ugonjwa wa ng'ombe, majipu, mvua ya mawe, nzi na giza
10. Farao alisema nini wakati kila tauni ilipokuwepo? Alisema nini Mungu alipotoa tauni?
Nitawaruhusu mwende Mungu akitoa tauni. Hapana hamtaenda.

Mistari ya kukariri

Jifunze orodha ya tauni zote kumi. Kutoka 3:4 – 6; Waebrania 11:24 – 25

Mazungumzo

Kumbuka ahadi alizopea Ibrahimu. Mungu alitimiza hizi ahadi namna gani wakati wa Musa. Mungu alimtarisha Musa kuwa kiongozi namna gani – kama mwana wa mfalme tena mchungaji.

Kuandika

Jifikirie kwamba wewe ni Mmisri wakati wa Musa. Andika juu ya tauni zilizokuja Misri. Andika vile kila tauni ilikuwa mbaya.

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 12 Musa akiwa Misri

SOMA Kutoka mlango wa 1 – 3

SOMO

Mungu aliahidi Ibrahimu ahadi kuu sana. Alirudia hizi ahadi kwa Isaka na kwa Yakobo. Mungu aliahidi kwamba wazao wa Ibrahimu watakuwa taifa kubwa. Wakati wa miaka ya njaa, Yakobo na familia yake walienda kuishi Misri kwa sababu Yusufu alikuwa na chakula chao cha kukula. Familia hiyo ilikaa Misri kwa miaka mingi mpaka ikawa taifa kubwa walioitwa Waisraeli. Walipoenda Misri walikuwa watu 70 kwa familia ya Yakobo. 📖 Soma Kutoka 1:7 inayotwambia vile waliongezeka na kua taifa kubwa.

Mungu aliahidi Ibrahimu na wazao wake nchi ya Israeli (Kanaani) milele. Lakini familia ya Ibrahimu sasa ilikuwa imekua taifa kubwa na walikuwa watumwa kwa nchi ya Misri. Kawaida Mungu hutimiza ahadi zake. Mungu alikuwa anaendesha mipango ili Waisraeli wasafiri na kurudi waishi kwa nchi yao aliyokuwa amewaahidi. Tutaona vile Mungu alitimiza ahadi hiyo.

Farao mwingine alikuwa mfalme wa Misri. Huyu Farao mgeni aliona kwamba hili taifa la Waisraeli kukua hivyo ilikuwa tisho kwa Wamisri. Wanaweza kuanza kupigana nao. Aliwafanya Waisraeli wawafanyie kazi kama watumwa. Alitaka wafanye kazi kwa nguvu



Hekalu za Misri

nyingi, wakitengeneza matofali ya kujengea miji na hekalu. Walitumiwa kikatili sana. Lakini Mungu alikuwa na watu wake, Waisraeli, na waliendelea kukuwa wengi. Farao alipoona Waisraeli wakiongezeka, aliamrisha kwamba watoto wavulana wa Waisraeli watupwe ndani ya mto.

Mwanamke mmoja Mwisraeli hakutaka mtoto wake afe. Alimficha kwa miezi mitatu. Alimweka kwa kikapu cha nyasi iliyopakwa lamu ili maji yasiingie ndani. Halafu akaiweka kando ya mto kwa unyasi. Dadake mkubwa wa yule mtoto alijificha ili aone kitakacho fanyika.

Bintiye Farao alikuja kwa huo mto ili aoge ndani ya hayo maji. Aliona yule mtoto na akamchukua. Dadake mtoto aliyekuwa akichunguza alikuwa na ujasiri sana. Alimuuliza kama angemtafutia mwanamke wa Kiisraeli ili amlindie. Binti Farao alipokubali, yule dadake alienda kuleta mamake.

Binti Farao alimwita yule mtoto 'Musa' kumaanisha 'tolewa kwa maji. Mama yake alimfundisha juu ya Mungu na ahadi zake kwa Waisraeli. Baadaye alipelekwa kwa nyumba ya Farao – jumba la mfalme. Musa akawa mwana wa mfalme kwa jumba la mfalme. Alikuwa na masomo mazuri ya juu na akajifunza kuwa kiongozi. Alikaa kwa jumba la mfalme mpaka akawa na umri wa miaka 40.

Lakini kwa wakati huu wote, Musa alijua yeye ni Mwisraeli sio Mmisri. Siku moja Musa alipokuwa mkubwa, alijaribu kutetea mtumwa, Mwisraeli. Aliua Mmisri aliyekuwa msimamizi wake. Mpaka Musa alikuwa atoroke. Aliondoka Misri na akatorokea Midiani na kuishi kule. Kule alikutana na familia ya mtu aliyetwa Yethro. Aliishi na hiyo familia ya Yethro akiwachungia kondoo. Musa alikuwa mchungaji kule Midiani kwa miaka 40. Wakati wote aliokuwa Midiani, alijifunza kuwa mvumilivu, kuishi kwa jangwa na kuwa mnyenyekevu.

Wakati huo huo, Waisraeli walikuwa wanateseka kule Misri. Farao aliwatumikia watumwa wake vibaya sana. Shida zao ziliongezeka. Walimlilia Mungu awasaidie. Mungu aliwasikiliza Waisraeli, watu wake. Mungu alikuwa anatarisha Musa kuongoza watu wake watoke Misri na warudi kwa nchi yao, Israeli yenye waliahidiwa na Mungu.

Siku moja, Musa alipokuwa Midiani akichungua kondoo, aliona jambo lisilokuwa la kawaida. Aliona kichaka kama kinawaka moto lakini hakikuwa kinateketea. Alipoenda karibu nacho kuangalia, alisikia sauti ikimnenea Mungu alikuwa anazungumza naye – Mungu wa babaye – Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Mungu alimwambia jina lake la kipekee - YHOVA maana yake MIMI NDIMI. Hii ilionyesha kwamba Mungu ni wa Milele. Yeye ni wa milele na milele. Mungu ako na watu wake wakati wote.



Mungu alimwambia Musa kwamba alikuwa amemchagua kuwaongoza watu wake Waisraeli kurudi kwa nchi yao aliyowaahidi. Mungu alimwambia Musa aende aambie Farao aachilie Waisraeli waende. Mungu alimwambia kwamba ataleta tauni kwa nchi ya Misri na itafanya Farao awaachilie waende.

Musa alirudi Misri. Haruni nduguye Musa alienda kumsaidia. Haruni na Musa walienda kwa Farao kumuuliza achilie Waisraeli watoke Misri lakini Farao alikataa kuwaachia waende. Farao alisema kwamba Musa analeta shida na Waisraeli waliowatumwa hawako kufanya kazi kwa bidii. Farao alikasirika. Aliamrisha Waisraeli wafanye kazi nyingi sana. Waisraeli walilia Mungu awasaidie.

Farao alifukuza Musa tena na Waisraeli walilalamikia Musa kwa sababu kazi ilikuwa imekuwa nyingi. Musa aliomba Mungu asaidie. Mungu alimwambia arudi tena kwa Farao. Musa aliambia Farao kwamba asipowaachilia Waisraeli waende, Mungu atageuza maji ya Mto wa Naili kuwa damu. Farao hakuwasikiliza. Kwa hivyo Musa akanyosha fimbo yake juu ya maji na maji yakageuka kuwa damu. Hii ilikuwa tauni ya kwanza kwa zote kumi zenye Mungu alileta Misri.

Mungu alituma Musa kwa Farao tena. Aliambia Farao kwamba asipowaachilia Waisraeli waende, kutakuwa na tauni ya vyura kwa nchi ya Misri yote. Farao alikataa kuwaacha Waisraeli waende. Bunde tu, nchi ilifunikwa kwa vyura. Vyura walikuwa kwa nyumba na kwa vitanda, vyungu vya kupikia na chini kwa miguu ya kila mtu. Farao aliita Musa na Haruni na akawaahidi kwamba atawaachilia Waisraeli waende akiwatoa vyura. Lakini baada ya Mungu kutoa vyura, Farao alibadilisha mawazo yake na hakuwaacha waende. Kila baada ya tauni hadi ya tisa, Farao alikuwa akisema kwamba atawaachilia Waisraeli waende. Lakini bunde tu Mungu alipotoa kila tauni, Farao alibadilika na kukataa kwamba wasiende. Hapo chini kuna orodha ya tauni zenye Mungu alileta kwa nchi ya Misri.

Wamisri waliabudu miungu wengi. Mungu alikuwa anaonyesha Farao na Waisraeli kwamba Yeye ni wa nguvu kuliko miungu wa Misri wowote. Wamisri waliabudu Mto wa Naili lakini Mungu aliigeuza kuwa damu. Waliabudu jua lakini Mungu aliifanya ikawa giza kwa siku 3.

Nchi ya Misri iliharibiwa. Mifugo wote walikufa. Mimea yote iliharibiwa kwa nzige na mvua ya mawe. Mungu alikuwa anaonyesha uwezo wake, lakini Farao alifanya moyo wake kuwa mgumu na kukataa kuwaachilia Waisraeli waende.

Katika somo lijalo, tutajifunza juu ya tauni ya mwisho. Hii ilikuwa mbaya sana mpaka Farao akawaachilia Waisraeli wakaenda.

Tauni kumi

1. *Maji ya mto iligeuka kuwa damu*
2. *Nchi ilijaa kundi la vyura*
3. *Nchi ilifunikwa kwa chawa*
4. *Kundi la mainzi*
5. *Ugonjwa uliua mifugo*
6. *Majipu yalikuja kwa watu na kwa wanyama*
7. *Mvua ya mawe iliharibu mimea*
8. *Tauni kuu ya nzige*
9. *Giza nene ilifunika nchi*
10. *Wana wazaliwa wa kwanza wote walikufa*